

iii- الإخفاء Al-Ikhfaa - Kuficha

Maana yake ni kuficha.

Katika hukmu za Tajwiyd ni kuificha nuwn saakinah au tanwiyn katika herufi za ikhfaa. Hivyo nuwn saakinah au tanwiyn itatamkwa ikiwa baina ya idhwhaar na idghaam kwa kuipa ghunnah isiyokuwa na shaddah.

Hukmu hii hutokea pale nuwn saakinah au tanwiyn inapofuatiwa na mojawapo ya herufi za ikhfaa:

ث ج د ذ ز س ش ص ض ط ظ ف ق ك

Itawajibika wakati huo kuificha nuwn saakinah au tanwiyn huku ikibakia ghunnah. Ghunnah ya ikhfaa hutegemea na herufi inayokuja baada yake kwa kuifanya kuwa tafkhiym (mdomo kujaa) au kwa kuifanya tarqiyq (mdomo usijae). Pia sauti ya ghunnah yake itabadilika kutegemea na makhraj ya herufi ya ikhfaa inayokuja mbele yake.

Herufi zake ni zile zote zinazobakia ukitoa herufi za idhwhaar, idghaam na iqlaab ambazo zimekusanyika katika mwanzo wa kila neno kwenye ibara ifuatayo:

صِفْ ذَا ثَنَاكُمْ جَادَ شَخْصٌ قَدْ سَمَا دُمٌ طَيِّبًا زِدْ فِي تَقَى صَعٌ ظَالِمًا

Ikhfaa inaweza kutokea katika neno moja au maneno mawili.

Namna ya kutekeleza ikhfaa:

Wakati wa kuificha nuwn saakinah au tanwiyn makhraj ya nuwn hubadilika kutoka kwenye ncha ya ulimi na kuwa karibu na makhraj ya ile herufi ya ikhfaa; kwa maana ya kuwa msomaji huweka ulimi wake mbali na makhraj ya nuwn na huwa karibu na makhraj ya herufi ya ikhfaa.

Mifano ya Ikhfaa:

Tanwiyn	Nuwn saakinah		Herufi
	Katika maneno mawili	Katika neno moja	
جَمَلَتْ صُفْرًا	أَنْ صَدُّوكُمْ	يَنْصُرُهُ	ص
فَاعِلٌ ذَلِكِ	عَنْ ذِكْرِ	فَأَنْذِرْ	ذ
مَاءٌ نَجَّاجًا	مِنْ ثُلْثِي	أُتِيَ	ث
وَرَزَقَ كَرِيمًا	أَنْ كَتَبَ	عَنْكُمْ	ك
فَصَبِرْ مِيلًا	مَنْ جَاءَ	نُجِجَ	ج
غِلَاطٌ شِدَادًا	مِنْ شَجَرَةٍ	وَأَنْشَقَّتْ	ش
شَاعِرٍ قَلِيلًا	مِنْ قَبْلِ	يَنْقَلِبُونَ	ق
قَوْلًا سَدِيدًا	عَنْ سَاقِ	الْإِنْسَانِ	س
ءَالِهَةً دُونَ	مِنْ دِينِكُمْ	عِنْدَ	د
صَعِيدًا طَيِّبًا	مِنْ طِينِ	يَنْطِقُونَ	ط
يَوْمَئِذٍ زُرْقًا	مَنْ زَكَّاهَا	أُنزِلَ	ز
مَاءً فَأَخْرَجْنَا	مِنْ فَوْقِكُمْ	أَنْفَطَرَتْ	ف
سُورَةً تُنَبِّئُهُمْ	لَنْ تَنْفَعَكُمْ	الْمُنْتَهَى	ت
مَعِيشَةً ضَنْكًا	مَنْ ضَلَّ	مَنْضُودٍ	ض
ظِلًّا ظَلِيلًا	مَنْ ظَلَمَ	فَلْيَنْظُرِ	ظ